



Namna ya Kuwa Salama Wakati wa Tetemeko la Ardhi

Ardhi inapotetemeka...


CHINI....



JKINGE....



SHIKILIA....





City of Seattle



Ofisi ya Usimamizi wa Matukio ya Dharura Seattle
www.seattle.gov/emergency
206-233-5076

Namna ya Kuwa Salama Wakati wa Tetemeko la Ardhi

- ★ Usikimbie wakati wa tetemeko.
Majeraha mengi hutokana na kuangukiwa na vitu na si majengo.
- ★ Kaa chini, jikinge na jishikilie chini ya dawati au meza kwa sekunde 3-4 za mtikisiko. Bakia hapo mpaka tetemeko liishe.
- ★ Iwapo upo katika sehemu isiyo na meza, kaa chini!
Fikiria chini, karibu, katikati.
Kuwa chini ya dawati au meza ni vema zaidi.
Kaa karibu na ukuta wa ndani.
Lala karibu na samani nzito.
Chuchumaa chini kati ya safu za viti ndani ya ukumbi wa sinema, kanisa au uwanja wa mpira.
Lala chini karibu au uvunguni mwa mikokoteni ya dukani.



- ★ Iwapo upo nje katika eneo la wazi...
Kaa chini na ujikinge kichwa chako kwa kutumia mikono.
- ★ Iwapo upo je karibu ya jengo...
Ingia ndani ya jengo na tafuta sehemu salama. Sehemu iliyopo karibu na jengo huitwa "eneo la hatari."
- ★ **KUMBUKA:** Milango SI sehemu salama wakati wa tetemeko. Ni vigumu kukaa mlangoni wakati wa mtikisiko na mlango mara nyingi husababisha majeraha unapofunguka na kujifunga nyakati za tetemeko.